# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# ZOEZI YA NYUMBANI 2026
# GREDI YA 5 - KISWAHILI LUGHA
# Muda: Saa 1 Dakika 40

### TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

### MAELEKEZO KWA WANAFUNZI

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu.

**Yohana:** (Kwa furaha) Shikamoo nyanya?

**Nyanya:** Marahaba mjukuu wangu. Umeshindaje?

**Yohana:** Nimeshinda salama, nyanya. Habari za utokako?

**Nyanya:** Kwema mjukuu wangu. Musa, mtoto wa mjomba wako ndiye aliyevunjika mguu alipokuwa akicheza na wenzake uwanjani.

**Yohana:** (Kwa huzuni) Maskini! Alipata msaada alipovunjika?

**Nyanya:** Huduma ya kwanza ni msaada unaompatia mtu aliyeumia au aliyezirai kumwepushia madhara zaidi. Hufanywa kabla ya kumpeleka hospitalini.

**Yohana:** (Kwa mshangao) Yeyote anaweza kutoa huduma ya kwanza?

**Nyanya:** La hasha! Walio na mafunzo ya namna ya kutumia vifaa kama bandeji, vitata, dawa ya kuua viini na vifaa vingine vinavyopatikana kwenye kijisanduku cha huduma ya kwanza ndio wanaoruhusiwa.

**Yohana:** Nitawaomba ruhusa wazazi wangu niende kumjulia hali Musa.

**Nyanya:** Utafanya vizuri sana.

**Yohana:** Nashukuru nyanya.

**Nyanya:** Tukutane kesho.

1. Mazungumzo haya yalifanyika wakati gani?

A. Asubuhi B. Mchana
C. Hatujajelezwa D. Jioni

2. Lengo la kumfanyia mtu huduma ya kwanza ni gani?

A. Kumpa majeruhi matibabu
B. Kumfurahisha majeruhi
C. Kuzuia madhara zaidi kabla ya kufikisha majeruhi hospitalini.
D. Kumponya mgonjwa badala ya kumpeleka hospitalini.

3. Ni jambo gani linaloonyesha kuwa Yohana ni kijana anayewajibika?

A. Anamjulia Musa hali.
B. Anaomba ruhusa kwenda kumjulia Musa hali.
C. Anajua kufanya huduma ya kwanza.
D. Anaaga nyanya yake kabla ya kuondoka.

4. Ni kifaa gani ambacho hakipatikani ndani ya kisanduku cha huduma ya kwanza?

A. Machela B. Pamba
C. Glavu D. Spiriti

5. Nyanya alipomwambia Yohana, tukutane kesho, Yohana angejibu namna gani?

A. Ya kuonana B. Inshallah
C. Buriani dawa D. Nawe pia

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Maadili ya Mosomi yalikuwa ya hali ya juu. Alikuwa barubaru mzuri aliyependwa na watu wote. Alikuwa kielelezo kwa wengi kijijini mwao na shuleni. Japo wazazi wake walikuwa maskini hohehahe, hilo halikumzuia kufanya bidii ya mchwa shuleni jambo lililomfanya kipenzi cha walimu na wanafunzi. Ungewasikia watu wengi wakisema kuwa wangependa kuwa na kijana mzuri kama Mosomi.

Mosomi alifaulu katika masomo yake. Bidii yake ilimfanya ajishindie zawadi tele. Msemo kuwa jina jema hung'aa gizani ulieleweka vizuri kwa Mosomi. Shuleni, Mosomi alipenda riadha akiwa katika gredi ya nne, alituzwa tuzo ya mwanariadha bora mwaka huo. Mosomi alikuwa duma katika mbio za mita mia moja. Tuzo hilo lilimfurahisha sana kiasi cha kutia bidii marudufu katika mazoezi yake. Anaamini kuwa juhudi ni pato. Talanta yake ilizidi kung'aa. Akaanza kushiriki mashindano makubwa makubwa. Hata ingawa wazazi wake hawakujimudu kumtimizia mahitaji yake mengi, mwalimu mkuu alimtafutia mdhamini ambaye alimsaidia kwa hali na mali.

6. Mosomi alikuwa kijana wa aina gani?

A. Maskini B. Mwadilifu
C. Mzembe D. Aliyependa msaada

7. Kwa nini Mosomi alipendwa na kila mtu?

A. Alikuwa na nidhamu na bidii.
B. Wazazi wake walikuwa maskini.
C. Watu walimhurumia hali yake.
D. Alifanya vizuri masomoni.

8. "Bidii yake ilimfanya ajishindie zawadi tele" ni methali gani inavyoweza kuelezea maneno haya?

A. Baada ya dhiki faraja.
B. Mtoto achekwaye ndiye mtoto.
C. Bidii hulipa.
D. Wema huozi.

9. Kifungu "......... hata ingawa wazazi wake hawakujimudu kumtimizia mahitaji mengi." kimetumiwa katika aya. Maana ya hawakujimudu ni

A. hawakupenda
B. hawakukataa
C. hawakuweza
D. hawakushindwa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Kuku aliondoka nyumbani kwake kwenda msituni kutafuta chakula. Kwa kuwa vifaranga wake walikuwa wachanga, hangewawacha nyumbani. Licha ya kuwa hakuwa na yeyote nyumbani wa kuwatunza wanawe. Walifika karasini, walimwona mwewe angani. Alimwamuru vifaranga wake warudi nyumbani wajifiche. Wote walimtii mama yao. Alishika njia kurejea nyumbani kwao. Dakika chache baadaye, mwewe alijitokeza njiani. Kuku walishika wayawaya. Alifuata mbio lakini maji yalikuwa tayari yameshagika. Mwewe alikuwa tayari amemnyakua kifaranga kimoja. Kilio cha kuku kwa kumwachilia mwanawe kiliambulalia patupu. Ama kweli, dua la kuku halimpati mwewe. Vifaranga wengine waliobaki walitoroka na kujificha msituni. Walishikwa na woga mwingi na wasijue la kufanya. Kuku aliwakusanya kwa jitihadi huku akitazama mwanawe akiingia fia kuchani pa mwewe. Kwa simanzi kuu alisema, "Hoidhuru, kuanzia leo tutakuwa waangalifu zaidi tukiwa njiani au mostakimuni petu."

10. Kwa nini kuku aliondoka nyumbani na vifaranga wake?

A. Walikuwa wakielekea barasteni.
B. Walikuwa na njaa.
C. Hakukuwa na yeyote wa kuachia vifaranga nyumbani.
D. Walikuwa wameenda kutafuta chakula.

11. Unafikiri kwa nini ilikuwa rahisi kwa mwewe kumnyakua kifaranga?

A. Vifaranga walikuwa wachanga.
B. Vifaranga hawakuwa na mwangalizi.
C. Vifaranga walikuwa na njaa.
D. Vifaranga walikuwa njiani.

12. Ni nani wa kulaumiwa kutokana na kisa hiki?

A. Kuku
B. Mwewe
C. Vifaranga
D. Kifaranga aliyenyakuliwa na mwewe.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Kuna mambo kadhaa yanayochangia umaskini. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na kukosa kazi na elimu. Mtu anaoaweza pia kuwa maskini kwa kufujiwa mali. Vilevile mtu akiwa mgonjwa kwa muda mrefu, hatakuwa na nguvu za kufanya kazi ilhali pesa nyingi zinatumiwa kwa matibabu. Watu wanao dai kuwa mtu anaweza kurithi umaskini wanakosa. Hakuna hali isiyoweza kubadilika. Hakuna jambo linaloweza kudumu milele.

Mbali ya kwanza ya kuukabili umaskini ni kujipatia elimu. Elimu hupanua mawazo ya mtu kuhusu namna ya kukabili maisha. Mtu aliye na elimu hakosi kazi na hata akikosa kazi ya kuajiriwa hujiajiri. Mtu akiwa na mtaji anaweza kuanzisha biashara ikanawiri hata akawaajiri wenzake. Akifanikiwa kwa hili, atakuwa amejisaidia yeye mwenyewe, jamii na nchi yake kuumaliza umaskini.

Kutumia vyema ulicho nacho ni njia nyingine ya kuukabili umaskini. Ukweli ni kuwa hakuna aliyezaliwa akiwa na mali. Matajiri wengi walijinyima raha na starehe maishani kwa minajili ya kuwekeza. Busara ya kutumia kidogo ulicho nacho ni kujiwekea msingi imara.

13. Ni jambo gani ambalo halichangii umaskini?

A. Ukosefu wa ajira.
B. Kukosa elimu.
C. Magonjwa ya muda mrefu.
D. Kurithi umaskini kutoka kwa wazazi.

14. Kifungu kimetaja njia ngapi za kuukabili umaskini?

A. Mbili B. Tatu C. Nne D. Tano

15. Maana ya kuwekeza kulingana na kifungu ni:

A. Kuweka pesa kwa matumizi ya baadaye.
B. Kuweka pesa kwenye benki.
C. Kutumia pesa katika biashara kwa lengo la kuzalisha zaidi.
D. Kutumia pesa kuendesha shughuli za kibiashara

16. Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Likizo ____ nilipata nyumbani kwao Paulina ____ Nilipofika, nilibisha lango kuu, ____ kwa heshima hadi sebuleni. Paulina akawasha runinga kisha tukaanza kutazama kipindi ____ tunakipenda sisi sote. Nilipoondoka jioni nikawaaga ____ wakanijibu binuru.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 16 | iliopita | iliyopita | lilipopita | niliopita |
| 17 | , | ! | : | . |
| 18 | nililekea | Nilielekeza | nilielekezwa | nilitelekezwa |
| 19 | ambaa | ambacho | ambaye | ambaye |
| 20 | alamsiki | kwaheri | buriani | usiku mwema |

Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi.

21.
22. Tambua nomino sahihi ya makundi.

A. Robota la maua.
B. Kipeto cha matunda.
C. Baraza la wanafunzi.
D. Matopa ya vitabu.

22. Tegua kitendawili: Shamba langu kubwa ila mavuno hayajazi kiganja.

A. Kichwa na nywele.
B. Mifupa ya samaki.
C. Miguu na njuja.
D. Macho na kope.

23. Kikomo kimetumikaje katika sentensi hii? Je, unamnjua Bi. Nyasuguta?

A. Kuonyesha kuwa sentensi imekamilika.
B. Kuuliza swali.
C. Kutenganisha maneno katika sentensi.
D. Kuonyesha ufupisho wa neno.

24. Nomino "nyakati" inapatikana katika ngeli gani?

A. U-ZI
B. I-ZI
C. I-I
D. LI-LI

25. Kisawe cha njia ni tariki. Je, kisawe cha bunda ni

A. chirimiri
B. hongo
C. kitita
D. mnyama

26. Kitenzi chora ni katika kauli ya kutenda. Kitenzi chenga katika kauli ya kutendana ni

A. chengea
B. chengana
C. changania
D. chengewa

27. Sentensi, "maisha yetu ndiyo huwavutia wanakijiji" ipo katika hali gani?

A. Tegemezi
B. Timilifu
C. Isiyodhihirika
D. Mazoea

28. Chagua udogo wa sentensi: Watu hao walikamatwa jana jioni.

A. Vijitu hivyo vilikamatwa jana jioni.
B. Majitu hayo yalikamatwa jana jioni.
C. Mtu huyu alikamatwa jana jioni.
D. Vitu hivyo vilikamatwa jana jioni.

29. Kamilisha methali: Bidii ya mja _______

A. huwa na mafanikio
B. hulipa
C. haiondoi kudura
D. haimchoshi mwanadamu

30. Chagua sentensi yenye nomino dhania.

A. Ukuta umepakwa rangi.
B. Mbwa koko anazururazurura mtaani.
C. Maji yakimwagika hayazoleki.
D. Mtoto ameshikwa na usingizi na kulala fofofo.

**MAJIBU**

1. D
2. C
3. B
4. A
5. B
6. B
7. A
8. C
9. C
10. D
11. B
12. A
13. D
14. A
15. C
16. B
17. D
18. C
19. B
20. A
21. D
22. A
23. D
24. A
25. C
26. B
27. D
28. A
29. C
30. D